# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS

TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA

## HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO

**MUHTASARI WA KIKAO MAALUM CHA CMT KUJADILI MPANGO WA UTEKELEZAJI WA MIRADI YOTE YA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA UVIKO 19 KILICHOFANYIKA TAREHE 21/10/2021 KATIKA UKUMBI WA MIKUTANO WA HALMASHAURI YA MJI MAKAMBAKO**

**Imeandaliwa na :-**
MKURUGENZI
HALMASHAURI YA MJI,
**MAKAMBAKO**

CamScanner

**WAKUU WA IDARA NA VITENGO WALIOHUDHURIA KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 21.10.2021**

| NA | JINA | WADHIFA |
|---|---|---|
| 1 | Kenneth K. Haule | Mkurugenzi wa Mji -Mwenyekiti |
| 2 | Norbetha Nyoni | Afisa Rasilimali watu na Utawala wa Mji - Katibu |
| 3 | Beatrice Tarimo | Kaimu Afisa Kilimo, Umwagiliaji na Ushirika wa Mji |
| 4 | Barnabas Slaqwara | Afisa Ugavi na Ununuzi wa Mji |
| 5 | Florensia Ngunangwa | Afisa Biashara |
| 6 | Baraka Manyangu | Kaimu Mkaguzi wa Ndani wa Mji. |
| 7 | Martin Mwallongo | Kaimu Afisa Mazingira na udhibiti wa taka ngumu. |
| 8 | Aderick Nombo | Afisa Elimu Sekondari wa Mji |
| 9 | Perpetua Masanja | Afisa Elimu Msingi wa Mji |
| 10 | Daktari Alexander Mchome | Mganga Mkuu wa Mji |
| 11 | Anna Mhoka | Afisa misitu |
| 12 | Samora Mgaya | Kaimu Afisa Mifugo na uvuvi wa Mji |
| 13 | Said Rajabu | Afisa Ushirika |
| 14 | Flaviana Mamkwe | Kaimu Afisa Ardhi na Maliasili wa Mji |



CamScanner

| | | |
|---|---|---|
| 15 | Eshter Mwakalindile | Afisa Utamaduni |
| 16 | Lina Sanga | Afisa Habari |

**MAHUDHURIO YA SEKRETARIETI YA KIKAO CHA CMT CHA TAREHE 21 OKTOBA 2021**

| | | |
|---|---|---|
| 1 | Albert Minja | Mwandishi wa Vikao |
| 2 | Mayanja D. Gava | Mwandishi wa Vikao |



CamScanner

Sekondari na Kassim M...

## AGENDA ZA KIKAO CHA CMT TAREHE 21.10.2021

1. Kufungua Kikao.
2. Kupokea agenda .
3. Utekelezaji wa Miradi ya Mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya Ugonjwa wa UVIKO 19.
4. Kufunga kikao.



CamScanner

## AGENDA NA 1/10/2020/2021 KUFUNGUA KIKAO

1.1 Mwenyekiti, kabla hajafungua kikao aliwasalimu kisha kuwakaribisha wajumbe katika kikao. Aidha, alifafanua kuwa amelazimika kuitisha kikao Maalum cha Kamati ya Wataalam kuweza kujadili na kwa pamoja kupanga mikakati ya namna ya utekelezaji wa Miradi ya maendeleo chini ya Mpango wa Maendeleo na ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO 19. Hivyo Mwenyekiti aliwataka wajumbe kujadili agenda za kikao kwa umakini.

1.2 Baada ya ufafanuzi huo Mwenyekiti alifungua kikao saa 10:22 jioni

## AGENDA NA 2/10/2020/2021 KUPOKEA AGENDA

2.1 Agenda nne (4) zilizoandaliwa zilisomwa kisha kuridhiwa na wajumbe ili zijadiliwe katika kikao.

## AGENDA NA 3/10/2020/2021 UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MPANGO WA MAENDELEO KWA USTAWI WA TAIFA NA MAPAMBANO DHIDI YA UGONJWA WA UVIKO 19.

3.1 Taarifa iliyohusu Halmashauri kupata Fedha za utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo chini ya mpango wa Maendeleo kwa ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya ugonjwa wa UVIKO 19 iliwasilishwa kikaoni kisha kujadiliwa na wajumbe kama ifuatavyo;-

3.2 **Majadiliano**

**3.2.1 ILIELEZWA** kwa Wajumbe kuwa Halmashauri ya Mji Makambako imepokea kiasi cha Tshs 1,140,000,000 katika mchanganuo ufuatao;- kiasi cha Tshs 520,000,000 za ujenzi wa madarasa 26 ya Sekondari kila chumba kwa gharama ya Tshs 20,000,000, Tshs 240,000,000/= ujenzi wa Shule Shikizi za Msingi 5 zenye madarasa 12 kwa kila moja, Tshs 80,000,000 kwa ajili ya ujenzi wa bweni la watoto wenye mahitaji maalum na kiasi cha Tshs 300,000,000/= kwa ajili ya ujenzi wa Majengo ya wagonjwa wa dharura.



CamScanner

3.2.3 **ILIFAFANULIWA** Kwa wajumbe kuwa utekelezaji wa Miradi hii inapaswa kufanyika haraka na kwa wakati ili kuendana na agizo la Mhe. Rais Samia Suluhu Hassan kuwa ifikapo Mwezi Januari 2022 madarasa yote yawe yamekamilika na pasitokee mtoto ambaye amechaguliwa kujiunga na kuingia kidato cha kwanza au darasa la kwanza amekosa nafasi ya kujiunga na Shule. Hivyo ili kuhakikisha kuwa utekelezaji wa miradi hiyo inafanywa kikamilifu mambo yafuatayo yalijadiliwa kisha kuafikiwa yafanywe kwa utekelezaji wa haraka;-

i. Shule zote za Msingi na Sekondari zilizopata Fedha zibainishwe na Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu wake wajulishwe kwenda benki kuangalia katika akunti zao na kutoa "bank statement", pia waandike kukiri mapokezi ya fedha hizo.

ii. Wakuu wa Shule na Walimu Wakuu waandikiwe barua kuwataka kuitisha vikao vya Bodi za Shule kwa Shule za Sekondari na Kamati za Shule kwa Shule za Msingi kuwataka kuunda na kuwasilisha kwa Mkurugenzi majina ya Wajumbe wa Kamati za Manunuzi ya vifaa, ujenzi , Mapokezi na ukaguzi wa vifaa, ikiwa pamoja na Mihtasari ya vikao vya Bodi na Kamati za Shule siku ya jumatatu ya tarehe 25.10.2021 kabla ya saa 9;30 alasiri.

iii. Walimu Wakuu na Wakuu wa Shule watangaze kazi haraka, Mafundi wapewe makadirio ya ujenzi "BOQ", na ramani ya ujenzi kwa mfano ule wa ujenzi wa madarasa ya Halmashauri ya Mji Handeni, Mafundi wapewe fomu na wakajaze bei "measurement" na kuziwasilisha kwa haraka.

iv. Kila Shule iwe na jalada la mradi ambalo litakuwa linahifadhi nyaraka

v. Iandikwe barua ya uteuzi wa Wajumbe saba wa ufuatiliaji wa Miradi ikihusisha wataalam ambao watawajibika katika majukumu mbalimbali kama ifuatavyo;- Eliud Mwakibombaki- Afisa Mipango Takwimu na ufuatiliaji wa Mji, Eunice Komba- Afisa Manunuzi na Ugavi wa Mji, Emily Maganga –Kaimu Mhandisi wa ujenzi wa Mji, Neema Chaula- Mratibu wa TASAF, Perpetua Masanja -Afisa ElimuMsingi, Aderick Nombo- Afisa Elimu



CamScanner

Sekondari na Kassim Mamba Afisa Mandeleo ya Jamii. Barua hiyo ifatanue hadidu za rejea kwa wajumbe ili waweze kutekeleza majukumu yao kikamilifu ikiwemo;- kufanya utafiti wa bei za Soko kwa bidhaa/vifaa vya viwandani kama vile saruji, matofali, bati,nondo, kufanya ufuatiliaji wa miradi yote ya maendeleo inayotekelezwa kwa fedha zote zilizokuja, Kutoa elimu kwa Kamati za ujenzi, Manunuzi, na mapokezi ya vifaa, Kufanya uhamisishaji wa jamii kuhusu mapokezi, utekelezaji na utunzaji wa miradi hiyo, kusimamia Sheria za manunuzi ya Umma wakati wa utekelezaji wa Miradi hiyo.

3.2.4 Baada ya majadiliano hayo wajumbe waliishukuru Serikali kuu kwa kuleta fedha za utekelezaji wa Miradi na kuahidi kuwa watasimamia kikamilifu utekelezaji wa miradi hiyo ili ijengwe kwa kasi na viwango na kuzingatia thamani ya Fedha.

**AGENDA NA 4/10/2020/2021 KUFUNGA KIKAO**

**4.1** **KABLA,**hajafunga kikao Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa ushirikiano walioonesha katika kujadili agenda za kikao kwa umakini **MWENYEKITI** alifunga kikao saa 11;45 jioni

**UMETHIBITISHWA LEO NA:-**

| | |
|---|---|
| **Saini**......Kenneth...... | **Saini**......[signature]...... |
| **Mwenyekiti** | **Katibu** |
| **Jina**..Kenneth..K...Haule | **Jina**..Norbetina...Nyoni |
| **Tarehe**..23/10/2022.. | **Tarehe**..22/10/2021.. |



CamScanner